**KISWAHILI - KIDATO CHA TATU**
**MTIHANI WA NUSU MUHULA**
**MUHULA WA KWANZA [FEB 2026]**

# MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

**SWALI LA KWANZA: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**

a) Taja aina mbili kuu za sauti za Kiswahili. (alama 1)
- ✓ **Konsonanti**
- ✓ **Irabu**

b) Taja aina mbili za ala za kutamkia kisha utolee mfano kwenye kila aina. (alama 2)
- ✓ **Ala tuli – ufizi, meno, kaakaa laini na gumu**
- ✓ **Ala sogezi – ulimi , midomo**

c) Unda neno lenye muundo huu: KKI – KI ( alama 1)
- ✓ **Mwana**

***Mwalimu akadirie jawabu la mwanafunzi.***

d) Maneno haya yako kwenye ngeli gani ? (alam 2)
i. Kiwete **A - WA**
ii. Chai **I - I**

e) Eleza matumizi matatu ya kistari kifupi kisha utolee mifano . (alama 3)
- ✓ **Kuandika tarehe 22-08-2022**
- ✓ **Kutenga silabi m-to-to**
- ✓ **Kutenga neno na maana yake. Baba – mzazi wa kiume.**

f) Tunga sentensi moja inayoleta dhana ya ombi/rai. (alama 1)
- ✓ **<u>Tafadhali</u> nieleze maana ya paa.**

g) Tia shadda kwenye neno lifuatalo ili kuleta dhana ya kasoro/dosari. (alama 1)
i. Walakini **wala'kini**

h) Tambua aina za maneno kwenye sentensi hii. (alama 3)

**Mtoto wa mwalimu alikuwa ameenda Nakuru.**

- ✓ **Mtoto – N**
- ✓ **Wa – V au H**
- ✓ **Mwalimu – N**
- ✓ **Alikuwa –Ts**
- ✓ **Ameenda – T**
- ✓ **Nakuru – E**

i) Tunga sentensi moja ili kutofautisha maana za maneno haya: ***kuku na gugu*** (alama 1)
- ✓ **Kuku- ndege wa jamii ya kanga anayefungwa.**
- ✓ **Gugu – mmea unaomea katika nchi kavu au msituni unaofanana na matete.**

**Mwanafunzi atunge mfano unaoafiki maana hizi**
**Mwalimu akadirie jawabu la mwanafunzi.**

j)
i. Eleza maana ya mofimu. (alama 1)
- ✓ **Kipashio/sehemu ndogo ya neno inayobeba maana na haigawiki zaidi.**

ii. Bainisha mofimu kwenye neno ***tumekutembelea*** (alama 3)
- ✓ **tu – kiima nafsi ya kwanza wingi**
- ✓ **me – hali timilifu**
- ✓ **ku – yambwa nafsi ya pili umoja**
- ✓ **tembe – mzizi**
- ✓ **le – kauli ya kutendewa**
- ✓ **a - kiishio**

k) Tambua aina za vielezi kwenye sentensi
i. Omondi alicheka kwa sauti. (alama 1)
**kwa sauti _ kielezi cha namna ala**
ii. Yohana alikimbia kiswara. (alama 1)
**Kiswara – Kielezi cha namana kimfanano**

l) Eleza matumizi ya ***na*** kwenye sentensi hizi.
i. Mucheru na mwalimu wake wataenda maktabani. (alama 1)
**na – kiunganishi kiongezi**
ii. Mwalimu Njau anaandika ubaoni. (alama 1)
**na – kiambishi cha wakati uliopo**
iii. Chakula kimepikwa na mama. (alama 1)
**Na – kihusishi cha kiima/mtenda**

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

m) Tambua aina za virai kwenye sentensi hii. (alama 3)

**Kiatu cha mwanafunzi kitashonwa kesho na fundi.**

- ✓ **Kiatu cha mwanafunzi – kirai nomino**
- ✓ **cha mwanafunzi - kirai kivumishi**
- ✓ **shonwa kesho na fundi – kirai kitenzi**
- ✓ **kesho na fundi – kirai kielezi**
- ✓ **na fundi – kirai kihusishi**

n) Taja aina zozote mbili za sentensi za Kiswahili. (alama 2)
- ✓ **Sentensi sahili**
- ✓ **Sentensi ambatano**
- ✓ **Sentensi changamano**

o) Changanua sentensi hii kwa masanduku/majedwali. (alama 4)

**Mtoto mdogo alikuwa ameumia sana lakini mama yake hakuwa amemshughulikia.**

| S | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| S 1 | | | | | U | S 2 | | | |
| KN | | KT | | | | KN | | KT | |
| N | V | Ts | T | E | | N | V | Ts | T |
| Mtoto | mdogo | alikuwa | ameumia | sana | lakini | mama | yake | hakuwa | amemshughulikia. |

p) Eleza maana ***tatu*** zinazojitokeza kwenye sentensi hii. (alama 3)

**Ahmed alimpigia Lincoln mpira**

- ✓ **Ahmed alimpiga Lincoln kwa sababu ya mpira.**
- ✓ **Ahmed aliupiga mpira kuelekea kwa Lincoln**
- ✓ **Ahmed aliupiga mpira kwa niaba ya Lincoln.**
- ✓ **Ahmed aliutumia mpira kama kifaa cha kumpiga Lincoln**

q) Nini maana ya msemo kula kalenda ? (alama 1) **fungwa jela.**

r) Tambua vishazi kwenye sentensi hii. (alama 2)

**Baisikeli iliyoibwa juzi ilipatikana jana.**

- ✓ **iliyoibwa juzi - Kishazi tegemezi**
- ✓ **Baisikeli ilipatikana jana – kishazi huru**

**SWALI LA PILI: ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

**Nipe chai,andazi mbili na egg moja...**

a) Taja sajili inayorejelewa na maneno haya.( alama 2)
- ✓ **Sajili ya hotelini.**

b) Fafanua sifa nane zinazohusishwa na sajili hii.( alama 8)
- ✓ **Matumizi ya msamiati maalum Kwa mfano chai,ugali,nyama,andazi**
- ✓ **Matumizi ya kauli fupi fupi Ili kuharakisha mawasiliano.kwa mfano nani mbuzi?**
- ✓ **Ukiukaji wa kanuni za kisarufi Kwa mfano chai mbili,ugali Moja**
- ✓ **Matumizi ya utohozi .Kwa mfano soseji**
- ✓ **Kuna matumizi ya kuchanganya ndimi Ili kurahisisha mawasiliano. Kwa mfano nipe chai na egg moja.**
- ✓ **Lugha ya heshima na unyenyekevu kutoka Kwa wahudumu Ili kuwavutia wateja.**
- ✓ **Matumizi ya lugha shawishi. Kwa mfano nunua chipsi na kuku upate soda Moja free.**
- ✓ **Lugha ya majibizano hutumika Ili kuyatambua mahitaji ya mteja.**

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes